JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS - TAMISEMI

Shule ya Sekondari ya Bukongo
S.L.P.474,
NANSIO-UKEREWE

19/05/2021

Simu:
Mkuu wa Shule Na 0756803560/ 0621632953
Makamu Mkuu wa Shule Na. 0758269165
Matron/ Na. 0769479484/0766777397
Unapojibu tafadhali taja
Kumb. Na BSS/S479/JI/FV/2021

Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi……
…….....
S.L.P…….
……..

Yah: <u>MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI BUKONGO HALMASHAURI YA WILAYA YA UKEREWE MKOA WA MWANZA MWAKA 2021/2022</u>

1. Nafurahi kukutaarifu kuwa, mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika shule hii kwa mwaka 2021/2022 kwenye tahasusi ya……. Shule ya Sekondari Bukongo ipo umbali wa Kilometa tatu (3km) Kaskazini mwa mji wa **Nansio.** Usafiri wa pikipiki au bajaji kutoka mjini Nansio unapatikana katika kituo cha pikipiki nansio au bandarini nauli ni shilingi **1000/=** kwa pikipiki na shilingi **2000/=** kwa bajaji.

   Muhula wa masomo unaanza tarehe 05/07/2021. Hivyo, mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe 05/07/2021. Mwisho wa kuripoti ni tarehe. 19/07/2021.

2. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA.

2.1 Sare ya shule

a) **Sare ya shule**; sketi **mbili (02) linda box** ndefu usawa wa kifundo cha mguu za rangi ya kijani iliyoiva. Shati mbili mikono mirefu nyeupe au nusu kanzu nyeupe (kwa waislamu).
b) Rangi ya hijab (kijuba) ni nyeupe.
c) **Sare ya michezo**; Track suit moja (01) rangi ya light blue na t-shirt moja rangi ya kijani iliyoiva isiyo na kola.
d) **Viatu vya shule;** vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi.
e) Soksi Jozi (pair) mbili nyeupe.
f) Sweta moja rangi ya kijani iliyoiva yenye shingo ya **V**;
g) T-shirt moja ya damu ya mzee yenye kola nyeusi;
h) Nguo za kushindia (*shamba dress*); gauni (mwamvuli) mbili ndefu hadi kifundo cha mguu kitambaa polista/tetron rangi ya light blue na isiwe sketi na blauzi.
i) Tai mbili za rangi ya pundamilia ya kijani iliyoiva na nyeupe;

2.2 Ada na Michango ya shule

a) Ada ya shule kwa mwaka ni shilingi **70,000.00** kwa mwanafunzi wa bweni. Ada inaweza kulipwa kwa kiasi cha shilingi **35,000.00** kwa muhula au kulipa ada yote kwa mara moja. Fedha hizo zilipwe kwenye Akaunti ya shule Na. **31403700129 Jina la account BUKONGO SEKONDARI** katika Benki ya **NMB**. (tafadhali andika jina la mwanafunzi na Kidato kwenye pay in slip).

b) Michango ya lazima inayotakiwa kulipwa na kila mzazi ni:-

i. Shilingi **15,000.00** kwa ajili ya ukarabati wa samani;
ii. Shilingi **6,000.00** kwa ajili ya kitambulisho na picha;
iii. Shilingi **20,000.00** kwa ajili ya taaluma;
iv. Shilingi **30,000.00** kwa ajili ya malipo ya wapishi, walinzi na vibarua wengine;
v. Shilingi **3,000.00** kwa ajili ya nembo ya shule;
vi. Shilingi **15,000.00** kwa ajili ya huduma ya kwanza yaani (Shilingi **10,000.00** huduma ya kwanza na Bima ya Afya shilingi **5,000.00**
vii. Pesa ya tahadhari **5,000.00** (haitarejeshwa).

c) Mahitaji muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuleta shuleni ni:-

i. Ream mbili 2 za karatasi kwa mwaka (**rimu A4 aina ya MONDI au DOUBLE A** –zinapatikana kwenye duka la shule.
ii. Daftari kubwa 8 counter books Q 3/4;
iii. Faili dogo la karatasi ngumu 1 (file folder)
iv. Kamusi ya kiingereza advanced oxford dictionary kunzia 7th edition na kuendelea;
v. Kalamu za wino (blue na nyeusi) penseli, rula, mkebe wa hisabati vinapatina kwenye duka la shule
vi. Mkoba wa mgongoni (bag) kwa ajili ya kubebea madaftari na vifaa vingine vya taaluma;
vii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika;
viii. *Dissecting kit* kwa wanafunzi wa Biolojia;
ix. Scientific calculator CASIO fx 991 kwa wanafunzi wa tahasusi za sayansi na biashara;
x. Godoro jipya la spongi ft. 2.5 la nchi 4;
xi. Mashuka pair 2 rangi light blue, blanketi 1, foronya 1, chandarua 1 pembe nne rangi ya bluu, taulo 1;
xii. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na Kikombe) na vifaa vya usafi binafsi (sabuni, mswaki, dodoki, dawa ya meno);
xiii. Ndoo mbili ndogo zenye mifuniko; na galoni 1 la lita 5 kwa ajili ya maji ya kunywa,
xiv. Krunzi au taa ya umeme wa jua kwa tahadhari umeme ukikatika (**LAZIMA**);
xv. Sanduku 1 la chuma kwa ajili ya kutunzia vifaa vyake.

d) Vifaa vya usafi;

i. Kwanja 1, jembe 1 na mpini wake, reki 1, mfagio wa ndani 1 na mfagio wa nje 1 kwa tahasusi za HKL na ECA.
ii. Kwanja 1, jembe 1 na mpini wake, brashi ya chooni 1, mopa 1 na mfagio mgumu 1 kwa tahasusi za CBG na PCB.

3. MAKOSA YATAKAYOSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE.

(i) Wizi.
(ii) Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro.
(iii) Kugoma na kuhamasisha mgomo.
(iv) Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/ walezi na jamii kwa ujumla.
(v) Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au na mtu yeyote.
(vi) Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika maarufu kama "Twende Kilioni" (ususi wa nywele ulionyooka kuelekea kisogoni matuta 5-7).
(vii) Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevya.
(viii) Uvutaji wa sigara.
(ix) Uasherati, uhusiano wa jinsi moja, kuoa au kuolewa.
(x) Kupata ujauzito au kutoa mimba.
(xi) Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi.
(xii) Kwenda kwenye majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni;
(xiii) Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule.
(xiv) Kudharau Bendera ya Taifa.
(xv) Kufanya jaribio lolote la kujiua, kuua au kutishia kujiua kama kunywa sumu n.k.
(xvi) Uharibifu wa mali ya Umma kwa makusudi.

4. VIMBATISHO NA FOMU MUHIMU.

a) Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa hospitali ya Serikali.
b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi/mkataba wa kutoshiriki katika mgomo, fujo na makosa ya jinai.
c) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni, kulipa ada, michango na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.
d) Picha nne (4) za Wazazi na Ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na namba zao za simu.
e) Nakala ya cheti cha kuzaliwa kilichothibitishwa.
f) Nakala halisi (original) na kivuli cha matokeo ya kidato cha nne.

g) Picha (2) passport size za mwanfunzi.
h) Fedha kama vile nauli ya kurudia nyumbani, fedha ya mtumizi madogo madogo, mzazi anashauriwa kumwekea kwenye akaunti yake benki au zitunzwe ofisi ya fedha ya shule na mwanafunzi atafunguliwa ukurasa wake wa matumizi na atasini kila anapochukua fedha. Hairuhusiwi mwanafunzi kukaa bwenini na kiasi cha fedha zaidi ya Tshs 10000/=

5. Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

KARIBU SANA KATIKA SHULE HII

SPECIOSA DEOGRATIAS KAPAMA
MKUU WA SHULE.

MKUU WA SHULE
BUKONGO SEKONDARI
S.L.P 474 NANSIO
UKEREWE

FORM Na –B

TAARIFA MUHIMU ZA MWANAFUNZI

Fomu hii ijazwa kwa usahihi na ukamilifu

A. TAARIFA ZA MWANAFUNZI
i.Jina……..Jinsi…….
Kidato…… Mchepuo…….Mwaka…….
ii. Tarehe ya kuzaliwa…….(siku/mwezi/mwaka)
iii. Anuani ya nyumbani…….
Iv.Mtaa/Kijiji anachotoka……Kata……Tarafa…….....
Wilaya…….Mkoa…….
v. Shule ya sekondari aliyotoka……
Anuani ya shule hiyo……
vi. Namba ya mtihani kidato cha nne……...
vii. Kabila…….
viii.Dini…….
ixUraia……..

B. TAARIFA ZA MZAZI

Bandika picha ya "passport" ya mzazi/mlezi HAPA

i. Jina la mzazi/mlezi……....(picha yake iko hapo juu)
ii. Anuani yake……...
iii. Namba ya simu…….
iv. Kazi/shughuli anayofanya……..
v. Kata…….Kijiji……Wilaya……
Mkoa……

C. NDUGU WA KARIBU
i. Jina……
Anuani……
Simu…….
Kazi anayofanya……
Uhusiano……

ii.Jina……
Anuani……
Simu…….
Kazi anayofanya……
Uhusiano

iii.Jina……
Anuani……
Simu…….
Kazi anayofanya……
Uhusiano…….....

D. TAMKO NA AHADI YA MWANAFUNZI

Mimi (jina)…….nakubali nafasi niliyopewa katika shule ya sekondari Bukogo. Naahidi kuwa nitazingatia taratibu, kanuni na sheria zote za shule. Nitafuata masharti yote yanayotolewa shuleni na viongozi wote wa shule. Pia ninahidi kushirikiana na wanafunzi wenzangu katika shughuli zote za shuleni kwa muda wote nitakao kaa shuleni. Kwa akili za timamu, taarifa zote nilizotoa ni sahihi na zinanihusu.
Jina……Sahihi…….Tarehe…….

TAMKO LA MZAZI

Mimi(jina)……nakili kuipokea na kuisoma kwa makini barua ya maelekezo ya mwanangu kujiunga na kidato cha tano katika shule ya sekondari Bukongo. Nakili kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo yote yaliyomo kwenye barua hii.
Ninaahidi kushirikiana na shule ili kuhakikisha mwanangu anapata haki yake ya elimu bila matatizo na kwamba nitatimiza mahitaji yote yaliyobainishwa katika maelekezo haya.
Jina…….Sahihi……Tarehe……

FORM Na.-C

UKEREWE DISTRICT COUNCIL
BUKONGO SEKONDARY SCHOOL
MEDICAL EXAMINATION FORM
(to be completed by a Medical Officer)

A. Student's Particulars

1. Student's name……Sex……..Age……..

2. Blood content (white and red)……

3. Urine……..

4. VD test……..

5. TB test……..

6. Chest test……..

7. Eye……

8. Spleen……..

9. Pregnancy test……..

10. Any additional information: for instance physical defects or chronic family diseases, etc

……

……

……

……

……

.....

.....

B. Medical Officer's Certification I certify that I have examined the above mentioned student and I recommend that she/he is fit/unfit to pursue A-level studies.

Name……..

Designation……

Signature……

Official Stamp……..

Date:…….